WAKINGE WAFANYIKAZI WA USAFIRI WA UMMA DHIDI YA MAAMBUKIZI YA HOMA YA COVID-19

MKATABA WA KIMATAIFA WA MATAKWA

Wafanyikazi wa usaifiri wa umma wako katika msitari wa mbele kwenye mapambano dhidi ya janga la Covid-19. Sisi ndio madereva, wauza tiketi, manamba, wahudumisha usafi, wahifadhi na wahudumu wa ofisi wanaotoa huduma muhimu zinazowezesha mifumo ya usafiri wa umma kufanya kazi – kuwawezesha wafanyikazi wengine muhimu kusafiri kwenda kazini na kuhakikisha kwamba wagonjwa wanahudumiwa na usambazaji wa bidhaa mbalimbali.

Zaidi ya 150 ya wafanyikazi wenzetu ulimwenguni wamefariki kutokana na maradhi ya Covid-19 wakati ambapo idadi ya visa vya maafa ikipanda kila uchao. Maelfu zaidi sasa wameambukizwa maradhi haya. Ukosefu wa kanuni za afya na usalama umezidisha hatari tunaokabiliana nayo tunapofanya kazi zetu muhimu wakati wa janga hili la Covid-19.

Kwa wafanyikazi wa usafiri wa umma, kama wafanyikazi wote muhimu wanaotarajiwa kuendelea kufanya kazi, hatari yetu ya kuambukizwa ni jambo la kuhusu afya na usalama kazini.. Kwa mujibu wa sheria za kimataifa, kunao ongezeko la jukumu la utunzaji. Nchi zingine tayari zinatambua maradhi ya Covvid-19 kama maradhi ya kikazi na wafanyikazi wastahili malipo ya fidia.

UKOSEFU WA KANUNI ZA AFYA NA USALAMA UMEZIDISHA HATARI UNAOWAKUMBA WAFANYAIKAZI WA USAFIRI WA UMMA WANAPOFANYA KAZI ZAO MUHIMU WAKATI HUU WA JANGA LA COVID-19

Lazima wafanyikazi wa usafiri wa umma wakingwe ipasavyo ili kuwawezesha kutekeleza kazi yao muhimu. Hakuna mfanyikazi ambaye anafaa ajihatarisha au kufariki kazini. Kama vile tumeshakuwa tukisema mara kwa mara, Shirikisho la Wafanyikazi wa usafiri wa umma (International Transport Workers' Federation-ITF) linasema kwamba wafanyakazi wa umma lazima wapate:

1. Vifaa bora vya kujikinga na vyakutosha

- Ikiwa ni pamoja na glavu, barakoa, vitakasa mikono na / au maji na sabuni
- Vilivyo na uwezo wa kuwakinga dhidi ya matone ambukizi hewani na maambukizo kupitia ngozi
- Na mpangilio unaofaa wa kufulia sare za kazi ili kupunguza maambukizi
- Na mafunzo yanayohitajika ya jinsi ya matumizi na kuvitupa baada ya matumizi
- Bila ya wafanyikazi kugaramia

2. Sheria za kazi ambazo zinapunguza usambazaji na kuwezesha watu kuweka umbali katikati yao, ikiwa ni pamoja na

- Kupata fursa ya kupimwa virusi vya Covid-19 bila ya ada
- Taratibu kali za kusafisha na kutakasa sehemu za ndani ya gari kila mara, mabweni na maeneo ya kazi, ikiwa ni pamoja na ofisi za tikiti na depo
- Kutokusanya nauli, malipo bila ya kutumia pesa taslim, kutokagua tikiti, kutumia mlango wa nyuma kuingia na / au kufunga mlango wa madereva (isipokuwa kwa abiria wenye ulemavu), vio salama za paspex, kuzuia utumiaji wa viti vya mstari wa mbele, kuruhusu idadi ndogo ya abiria garini, kuweka kipaumbele wafanyikazi muhimu, utoaji wa barakoa kwa abiria, malipo ya mikopo kusitishwa kwa muda na kuondolewa kwa malengo ya mapato
- hatua salama za kusafiri kwa wafanyikazi wa usafiri wa umma wakati ambao vizuizi vya kusafiri vipo
- Vituo zaidi vya kujisaidia na kupumzika kwani kunao upungufu wa vyoo vya umma na vifaa vya kuoga na kule kuzingatia kuzuia mkusanyiko wa watu wengi kunasababisha mwendo wa polepole
- haki ya kujiondoa katika hali ya kazini ambayo uhatarisha maisha au afya zao, bila hofu ya kuchukuliwa hatua

3 Hatua za kiafya zinazowalinda walio hatarini na wagonjwa, pamoja na

- mshahara wa kutosha na hakikisho la ajira kwa wafanyikazi ambao wangejitenga kwasababu ya hatari zinazojulikana kwao na/au jamii yao zikiwemo shida za kiafya na ujauzito
- bima ya afya ya kudumu inayojumuisha huduma ya ugonjwa wa akili
- likizo ya kulipwa ya kutosha na fidia ya kifedha kwa wafanyikazi walioadhirika kwa ugonjwa wa Covid-19 kibinafsi au jamaa zao (kwa mfano maambukizi, kujitenga au jukumu la kutunza watoto)

4. Utambuzi wa jukumu muhimu ya wafanyikazi wa usafiri wa umma, pamoja na

- Nyongeza ya ujira au mapato
- kazini / fidia na faida katika tukio la kifo, ikiwa ni pamoja na malipo ya baada ya kustaafu

5. Habari na ripoti za mara kwa mara kuhusu za hatari kazini na afya ya wafanyakazi, pamoja na

- utoaji wa habari kwa haraka na mafunzo ya kutosha juu ya hatua wanazochukua waajiri kukabiliana na homa ya Covid-19 ili kubaini hatari, mwelekeo wa hatari ya maambukizi na athari za kiafya
- Idadi ya ya wanaojitenga, maambukizi na vifo, kulingana na jinsia, kabila, asili na aina ya kazi ili kuhakikisha utofu wowote wa usawa unawezachunguzwa na kukabiliwa
- Na mbinu mwafaka za kuwasilisha malalamiko zinazowalinda wapiga filimbi zinzaowawezesha wafanyakazi kuripoti hatari bila kujulikana ikiwa mapenzi yao, bila woga wa matokeo ya baadae

6. Haki za mashirika za wafanyikazi, ikiwa pamoja na:

- mashauriano na ushiriki katika muundo wa utenda kazi, michakato na hatua zote za kiafya na usalama
- hatua za kuwezesha uwakilishi wa wafanyikazi katika sehemu za kazi na kwa umbali kwa wafanyikazi wailo mbali au wamejitenga

Hatua hizi lazima zitumike kwa wafanyikazi wa umma wote, bila kujali majukumu yao, mpangilio wa kandarasi na hali ya ajira na kuwajibika kwa jinsia zote na hali ya uhamiaji.

Shirikisho la Kimataifa la wafanyikazi wa usafiri (The International Transport Workers' Federation-ITF} pia linaunga mkono mwito kwa washonaji wa maazi ulimwenguni kulinda mapato ya wafanyikazi, afya na ajira kwa wafanyikazi wanaotengeneza vifaa vya kujikinga binafsi, kuambatana na kanuni za mkataba huu.